MWONGOZO WA NOVELA

"UTEUZI WA CHALE "-Asumpta K Matei.

Mwalimu Sudi.G.Hamisi

Mwalimu Mzoefu na mwenye tajriba pana katika uwanja wa Jiografia/ Kiswahili lugha na fasihi.

B.E.D /Arts MOI UNIVERSITY.



MUKHTASARI.

Uteuzi ni neno linalotokana na neno teua yaani chagua.Chale ni mhusika katika novela hii.Uteuzi wa Chale ni uamuzi ambao mhusika chale alipaswa kuchukua katika kuchagua kipawa kipi angetumia ili kuitumikia jamii.

Chale ambae ni mwanafunzi wa gredi ya saba anafahamika Kwa umaarufu wake kutokana na kipaji chake cha utangazaji.Yeye hutangaza au hupeperusha matangazo ya michezo ya vijana wanapokuwa wakijumuika pamoja katika michezo hiyo na kuifanya kufana zaidi na yenye mvuto.Wanapokuwa katika mashindano ya kuogelea katika bwawa la Mpingoni,yeye hupeperusha matangazo ya mashindano hayo ya kuogelea akiwa kwenye jiwe maarufu lililofahamika kama 'Sanduku la mtangazaji'.Aliyapamba mashindano haya nakuyafanya yakuvutia zaidi hadi baadhi ya vijana wenzake wakambandika jina "mtangazaji mtarajiwa".

Siku moja Chale na wenzake wakiwa wametekwa na shughuli za mashindano ya uogeleaji,walijisahau kuwa walifaa kuwatupia jicho ng'ombe na hivyo basi,ngombe hao wakatokomea walikokwenda.Ghafla bin vu walilingundua hili na Ili kuepuka adhabu watoto wenzake wakapiga lundi.Chale alimuona baba yake amefika bwawani lakini hakudhihirisha sura ya hasira.Mbali na hivyo Chale alivaa gwanda lake na kutoka shoti mithili ya risasi.

Edit with WPS Office